



Mbuzi hawa wamefungwa na chakula kimening'inizwa juu ya mti

Uchungaji wa mbuzi kwa njia ya kufunga kamba kwenye mti au kigingi unatumika sana maeneo mengi barani Afrika. Tanzania yenyenye jumla ya mbuzi takribani millioni 15 (sensa ya 2008) wakiwa wanafugwa na wafugaji wadogo wanafuga mbuzi kwa njia kuwafungia ndani na kuwalettea chakula, wengine wanawapeleka mbuzi malishoni mchana na wengine wanawafunga kwenye miti au vizingi. Utafiti uliofanywa na mradi uliokuwa chini ya Davies (1993-96) mkoani Morogoro katika vijiji vyta Mgeta, Mlali na Melela ulionyesha kuwa njia kuu ya ufgaji Mgeta ilikuwa ya kuwafunga mbuzi, wakati mlali walikuwa wakitumia ya kuwafunga mbuzi wakati wa mvua na ni kwasababu ya ukosefu wa watu wa kuchunga mbuzi kwani huwa kwenye shughuli za kilimo.

Kasi ya matumizi ya kufunga mbuzi kwenye malisho imeongeza kasi yake miaka ya karibuni kutokana na ukosefu wa watu wa kuwachunga mbuzi. Watoto wanaenda shule wakiwa bado wadogo, na pia watoto wengi sasa hawataki kufanya kazi ya kuchunga kutokana. Njia rahisi kwa wafugaji wa mbuzi wanaona ni kuwafunga eneo lenye malisho na kuwaacha hapo. Njia hii hutumika zaidi wakati wa mvua ambapo wafugaji hujikita zaidi katika shughuli za kilimo na hivyo kukosa mtu wa kuchunga.

Tafiti pia zinaonyesha kwamba wafugaji wamekuwa wakiwafunga mbuzi malishoni na kuwaacha huko wengine wanawafunga kwa muda mfupi wakiamini kuwa mbuzi

watakula haraka haraka na kushiba. Tena wamekuwa wakiwafunga mbuzi katika eneo moja kwa siku mbili au zaidi huku kila siku wakiongeza urefu wa kamba. Wafugaji wengi wamekuwa wakiwafunga kamba jirani na nyumbani sehemu yenyе majani ya kutosha kwa ajili ya usalama pia.



Mbuzi hawa hawajafungwa kwenye mti bali mchungaji ndiye ameshika kamba na hivyo huwahamisha toka sehemu moja kwenda nyingine kadri aonavyo inafaa

Mambo ya kuangalia kabla ya kumfunga mbuzi malishoni

1. Eneo unalofunga mbuzi liwe chakula ambacho mbuzi wanapenda kula na kiwe cha kutosha
2. Hakikisha kama si ndefu sana hasa lakini kipenyo chake kiwe na cha kumfanya mbuzi ashibe
4. Sehemu unayomfunga mbuzi iwe na kivuli cha kumkinga na jua kali
5. Sehemu unayomfunga pasiwe na miti mingi karibu kuzuia mbuzi asijiviringishe na kuleta madhara
6. Sehemu unayomfunga mbuzi kusiwe na wanyama wanaoweza kumdhuru mbuzi kama nyoka na mbwa
8. Ni vema kumfunga mbuzi kwa muda usiopungua 6-8 ale apate chakula cha kutosha
9. Kumbuka kumpa maji ya kunywa

Madhara ya ufugaji wa kufunga mbuzi malisshoni

Tafiti ambazo zimefanywa zinaonyesha kuwa ufugaji wa aina haina hauna madhara kwenye ukuaji wa mbuzi kama kanuni na taratibu zitazingatiwa hasa uhakika wa

upatikanaji wa chakula katika eneo alilofungwa mbuzi. Madhara yanayoweza kujitokeza ni kwa mbuzi kujiviringisha kwenye kama kunakoweza kupelekea kifo cha mbuzi. Hivyo kamba inapaswa isiwe ndefu sana na eneo analofungwa kuiwe na miti mingi na zaidi chakula cha kutosha kiwepo katika eneo alilofungwa tena chenye mvuto sawia. Mbuzi anaweza kuumwa na mbwa au nyoka na kusababisha kifo